BAJUNI

# MWONGODHO WA MWALIMU
# GIREDI 1

Yumna Hamid Titi
Fuad Aroi
Yumbe Athman

TWAWEZA COMMUNICATIONS
Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association
Umoja ni Nguvu

SWAHILI RESOURCE CENTRE
Old Town, Sir Mbarak Hinawy Road, Mombasa

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nḏa Twaweza Communications
Chapisho la Kwanḏa 2024

**ISBN: 978-9966-128-19-5**

Kitabu cha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Nradi huu huṯekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na Department for Digital, Culture, Media and Sport.

In partnership with

BRITISH COUNCIL

Department for Culture, Media & Sport

# Yaliyomo


1. N̠umbani Kwechu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

2. Sikuli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

3. T̠abia Nd̠uri . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 11

4. Afiya – Uswafi wa Nvili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 17

5. Nyakati na Dhipindri. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 22

# SHUKURANI

Dhiṯabu dha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Chwatoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuanḏika na kuchapisha dhiṯabu hidhi. Bila nsaada wavo ingalikuva ṯabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a kuifundrisha kusoma na kuanḏika Kibajuni. Chwavashukuru Dkt. Rukiya Harith na Nafisa Awadh kwa ushirikiano wavo na vaanḏishi kachika haṯua dhoṯe dha kuanḏika nfulululidho wa *Chusomeni Kibajuni*. Vaandishi va dhiṯabu hidhi – Yumna, Aroi na Yumbe – valiiṯolea kushiriki na kumalidha kuanḏika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia twavashukuru vale voṯe chufanyao navo kadhi hii adwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni.

Kimani Njogu, Twaweza Communications
Omar Lali, Shungwaya Welfare Association
Athman Lali Omar, Swahili Resource Centre

Novemba, 2023

# 1 ṈUMBANI KWECHU

**ISOMO LA KWANḎA**

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: KUANḎAMA MAAGIDHO**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuanḏama maagidho ṯafauti ahusianao na shuhuli dha ṉumbani

(b) Kuṯaba shuhuli mbalimbali dha ṉumbani

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 1

**Dhifaa dha Kufundrishia**: dhifaa halisi, kadi maneno

**Swali ḏaḏisi**: Kwa nini kuanḏama maagidho ni muhimu?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi kujaḏili na kudhichambua picha dhilidhoko kweṉe kiṯabu cha mwanafunḏi uk. wa 1.
- Kuchaya maina a dhifaa halisi na kueledhea machumidhi ake ṉumbani.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kuchaya shuhuli mbalimbali dha ṉumbani.

**ISOMO LA PILI**

**MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA**

**MAḎA NDRODI: SALAMU DHECHU**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuchumia nsamiaṯi halisi wa salamu.

(b) Kusalimiana kulingana na wakaṯi wa siku na umuri wa nchu.

(c) Ave na madhovea a kusalimiana.

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 2

**<u>Dhifaa dha kufundrishia</u>**: kadi maneno, kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi** – Vachu husalimianaye Kibajuni?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kuchaya salamu mbalimbali
- Vashuhulishe vanafunḏi kujadili nchoro kachika kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 2.
- Kuvaongodha vanafunḏi kusoma salamu mbalimbali dhilidhoko kiṯabuni
- Vakiva vavili vavili vanafunḏi vatabe salamu mbalimbali

## ISOMO LA CHACHU NA LA IṈE

## MAḎA KURU: KUSOMA

## MAḎA NDRODI: KUSOMA SAUṮI DHECHU

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuṯamuka silabi dha sauṯi dhechu

(b) Kuchambua silabi dha sauṯi dhechu

(c) Kusoma ngano kwa kufululidha.

**Swali ḏaḏisi**: Ni dhifaa dhipi dha ṉumbani udhiivadho?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 3

**Dhifaa dha kufundrishia**: Dhifaa halisi, kadi maneno

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kuvaongodha vanafunḏi vachaye harufu dhoṯe dha alfabeti.
- Vaekedhe vanafunḏi vasome silabi kachika kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 3.
- Vaṯankie sauṯi hidho ili vakariri baada a mwalimu.
- Vaongodhe vanafunḏi kuchambua silabi dha sauṯi hidho.
- Vaangalie picha na vachaye vakivonacho.
- Vaongodhe kusoma nganu kwa sauṯi.
- Vavulidhe maswali vajibu kwa ndomo.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: SHIKANISHA SILABI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kushikanisha silabi kupacha ineno sawa

(b) Kuchumia silabi na kusoma ineno

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk wa 4

**Dhifaa dha kufundrishia**: dhifaa halisi, kadi-maneno, kifaa cha kidijitali

**Swali ḏaḏisi:** Je ni dhichu gani chwawedha kupacha ṉumbani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi ni dhichu gani dhipachikanadho ṉumbani
- Vavoneshe dhifaa halisi na vachaye maina a dhichu hidho.

- Vaekedhe kachika kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 6.
- Vachaye na vaanḏike maina adhifaa hidho.
- Vaongodhe vanafunḏi kukamilisha dhoedhi.

**Majibu alopenḏekedhwa**

a) Medha b) kisu c) Kichi

1. Mwakisu
2. Muti
3. Kibakuli
4. Uteo
5. Upeo

**ISOMO LA SIṮA**

**MAḎA KURU: KUANḎIKA**

**MAḎA NDRODI: DHICHU DHA ṈUMBANI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**

**Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe**

(a) Kuchaya maina a dhichu dha ṉumbani

(b) Kuchambua machumidhi a dhichu dha ṉumbani

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 5

**Dhifaa dha kufundrishia:** dhifaa halisi, kadi-maneno, dhifaa dha kidijitali

**Swali ḏaḏisi**: Dhifaa dha ṉumbani dhina umuhimu gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi dhifaa dhipachikanadho ṉumbani.

- Vaekedhe vanafunḏi kweṉe ukurasa wa tano
- Vaongodhe vanafunḏi kuchaya maina a michoro ilioko kiṯabuni
- Vaongodhe kachika dhikundri vachaye maina a dhichu dha ṉumbani.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. jambi
2. itasa
3. ndroo
4. kifumbu
5. kibahalulu
6. upeo

# 2 SIKULI

**ISOMO LA KWANḎA**

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: KUUNDRA MANENO**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

I. Kuṯanka silabi kweṉe maneno

II. Kutanganya silabi apache ineno.

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. wa 8

**Dhifaa dha kufundrishia**: dhifaa halisi, kadi-maneno

**Swali ḏaḏisi:** Ineno huundrwae?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha kipindri kwa kuvaambia vanafunḏi vachaye harufu dhote dha alfabeṯi.
- Vaongodhe kuṯanka silabi hidho.
- Vaongodhe vanafunḏi kudhiṯanganya silabi kupacha ineno sawa.
- Vahimidhe vanafunḏi kuchambua silabi na kudhiṯanganya kupacha ineno sawa.

**ISOMO LA PILI**

**MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA**

**MAḎA NDRODI: KUANḎAMA MAAGIDHO**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe

(a) Kuanḏama maagidho alopawa

(b) Kufurahia kuanḏama maagidho a sikuli

**Swali ḏaḏisi**: Kwa nini ni muhimu kuanḏama maagidho?

**Dhifaa dha kufundrishia**: Dhifaa halisi, chati

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa 7

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha kwa kuvavulidha maswali mbalimbali kuhusu sikuli.
- Vaongodhe vanafunḏi kujadili michoro ilioko kiṯabuni ukurasa 8 kimakundri.
- Vashirikishe kujaḏili michoro kwa pamoya.
- Vaongodhe kuchora benḏera na kuipaka rangi.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

## MAḎA NDRODI: KUSOMA SAUṮI NA SILABI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuchambua sauṯi ihusianao na madhingira a sikuli.

(b) Kusoma ineno lihusianalo na madhingira a sikuli

**Swali ḏaḏisi:** Ineno husomwae?

**Dhifaa dha kufundrishia:** kifaa cha kidijitali, kadi-maneno

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 8.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**:

- Changulidha kwa kuimba wimbo uhusianao na madhingira a sikuli
- Vasikidhishe sauti mbalimbali ukichumia kifaa cha kidijitali.

- Vaongodhe vanafunḏi vachaye maina a michoro kachika kiṯabu cha mwanafunḏi uk 8.
- Mwanafunḏi asome sauṯi dhilidhoko kweṉe jedwali baada a mwalimu.
- Vaongodhe kusoma silabi ili vapache maneno sawa.

**ISOMO LA IṈE:**

## MAḎA KURU: KUSOMA

**MAḎA NDRODI: KUSOMA MANENO**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

(a) Kusoma maneno kwa matanshi bora

(b) Kuchunga senchensi kuchumia maneno.

**Swali ḏaḏisi:** Maneno husomwae?

**Dhifaa dha kufundrishia**: Kadi-maneno, kifaa cha kidijitali.

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa 9

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha isomo kwa kuvavonesha vanafunḏi kadi maneno ili vadhisome.
- Vaongodhe vafungue kitabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 9, vasome maneno kwa sauṯi, mwalimu atoe mifano a senchensi, vanafunḏi varudie senchensi hidho.
- Vaongodhe kuchunga senchensi kuchumia maneno valopawa.

## ISOMO LA ṮANU:

**MAḎA KURU: KUANḎIKA**

## MAḎA NDRODI: HAṮI NḎURI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe.

(a) Kuanḏika senchensi kwa haṯi nḏuri

(b) Kufurahia kuanḏika senchensi kwa haṯi nduri

**Swali ḏaḏisi**: Haṯi nḏuri ni gani?

**Dhifaa dha kufundrishia**: Chati

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 9.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Vaongodhe kuanḏika harufu hewani.
- Vavoneshe chati eṉe maanḏiko madhuri
- Vaongodhe kuvavonesha harufu dheṉe mikia a iyu na a ṯini, na dhilee dha kachikachi.
- Vaongodhe kusoma senchensi, kiṯabu cha mwanafunḏi uk wa 9
- Vaangodhe kudhianḏika senchensi hidho kwa haṯi nduri.

## ISOMO LA SIṮA

**MAḎA KURU: KUANḎIKA**

## MAḎA NDRODI: MANENO MAPIYA

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe.

(a) Kuyadha pengo kuchumia silabi sawa

(b) Kufurahia kuanḏika maneno kwa udhuri

**Swali ḏaḏisi**: Haṯi nduri ni gani?

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi-maneno, kifaa cha kidijitali

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Vaongodhe kwa kuvavonesha picha ulidhodhiṯayarisha
- Vavulidhe maswali elekedhi vawedhe kuchambua nomino hidho.
- Vambie vafungue kitabu cha mwanafunḏi uk 9
- Vaongodhe kujibu maswali hao.
- Fanya marudio na vanafunḏi

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. Saa
2. Medha
3. Kifuchio
4. Kichi
5. Kiṯabu

# 3 ṮABIA NḎURI

**ISOMO LA KWANḎA**

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: NGANU**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kusikidha nganu na kufurahia.

(b) Kuchambua maneno a heshima na tabia nḏuri.

**Swali ḏaḏisi**: Nganu husaidia nini?

Nganu hutolewa na nyani na wakati gani?

**Marejeleo:** Kitabu cha mwanafunḏi uk. wa 10.

**Dhifaa dha kufundrishia**: dhitabu dha nganu.

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Mwalimu avapange vanafunḏi tayari kusikidha nganu. Mwalimu ahakikishe vanafunḏi vote hunvona kwa udhuri.
- Mwalimu avasimulie nganu huku akikariri maneno a heshima kwa kurudiarudia.
- Mwalimu avavulidhe vanafunḏi maswali kutoka kwa nganu valosikidha.
- Mwalimu avahimidhe vanafunḏi kuchaya maneno a adabu kuṯoka kwa nganu.
- Vanafunḏi vasome maneno a adabu ubavoni
- Mwalimu avapongedhe na kuvapa kadhi a dhiada.

**Kadhi a dhiada**

Ukendra n̠umbani mwambie ndhadhi akusimulie nganu ifundrishao tabia nduri.

**ISOMO LA PILI**

## MAḎA: KUDHUNGUMUDHA

**MAḎA NDRODI: MANENO A ṮABIA NḎURI**

**Maṯokeo maalumuuu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuṯaba salamu

(b) Kuchumia salamu kwa usawa na kufurahia

**Swali ḏaḏisi**: Uṯan'yivaye mwana mwene adabu?

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 10

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi-maneno, kadi maneno, chati ya salamu na majibu

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Mwalimu avaavanye vanafunḏi kachika dhikundri. Vaamrishe vakumbusane maneno a aḏabu valosoma kachika nganu somo lililopicha.
- Mwalimu avasaidie vanafunḏi kusoma maneno a ṯabia nduri ubavoni
- Vanafunḏi vasome mifano dhiṯabuni
- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi kutukua kadi dhen̠e maneno a adabu
- Kachika dhikundri vanafunḏi vaambiane maneno a tabia nduri.
- Mwalimu avapongedhe vanafunḏi na avahimidhe kuchumia maneno a adabu n̠umbani.

## ISOMO LA CHACHU

### MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: MANENO NA SENCHENSI DHA AḎABU

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kusoma senchensi kwa ufasaha

(b) Kuchambua maneno a adabu na ṯabia nḏuri

**Swali ḏaḏisi**: Ni maneno gani chuchumiao a adabu?

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk 11

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi-maneno, chati

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Vakiva kachika dhikundri, vanafunḏi vakumbusane maneno a ṯabia nduri
- Mwalimu avaanḏikie vanafunḏi silabi vasome kwa sauṯi
- Mwalimu achumie kadi dha maneno, vanafunḏi vasome. Vashirikishe vanafunḏi kuunganisha kadi dha maneno kuchunga senchensi
- Hatimaye vanafunḏi vasome senchensi kwa sauṯi.

## ISOMO LA IṈE

### MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: NGANU

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kusoma nganu kwa udhuri

(b) Kuṯauwa maneno a tabia nduri kuṯoka kwa nganu

(c) Kujibu maswali kuṯoka kwa nganu

**Swali ḏaḏisi**: Kwa nini tuve na tabia nḏuri?

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa 11

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi-maneno

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**:

- Changulidha kipindri kwa maswali kuhusu ṯabia nduri
- Vaongodhe vanafunḏi kusoma hadisi na vachambue maneno a ṯabia nduri.
- Vanafunḏi vasome hadisi kwa umakinifu sana. Chilia nkadho maneno a ṯabia nduri
- Vape nafasi baadhi a vanafunḏi vasome kwa sauti.
- Vashirikishe vanafunḏi kuchunga senchensi vakichumia kadi-maneno.
- Hitimisha kipindri kwa kuvaagidha vanafunḏi vajibu maswali.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Mwana ndhuri
2. Hunena asanta
3. Huomba radhi

**ISOMO LA ṮANU**

**MAḎA KURU: KUANDIKA**

**MAḎA NDRODI: IMLA**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuandika maneno sawasawa kwa kusikidha

(b) Kuandika kwa udhuri

(c) Kufurahia kuandika

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafundi ukurasa 12

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi-maneno, michoro

**Swali ḏaḏisi**: Kusikidha kwa makini husaidia nini?

Kwa nini hufanya imla?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avatayarishe vanafunḏi kwa isomo.
- Mwalimu ahakikishe kila mwanafunḏi unao kalamu na kiṯabu/buku.
- Mwalimu avape vanafunḏi maagidho a kuva makini na kusikidha.
- Mwalimu asome maneno kwa utaratibu kwa kudhingatia silabi kwa kuendreledha.
- Mwalimu adhunguke darasani kuhakikisha vanafunḏi vote huandika anenao.
- Vavoneshe vanafunḏi kadi- maneno ambao vameaandika.
- Vape muda baadhi a vanafunḏi vaitokedhe ivo veneve kusoma maneno valoandika
- Vanafunḏi varekebishe kadhi dhavo.

**ISOMO LA SIṮA**

**MAḎA KURU: KUANḎIKA**

**MAḎA NDRODI: PANGA HARUFU UPACHE INENO LILO SAWA**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafundi awedhe:

(a) Kuunganisha silabi kupacha ineno lilo sawa.

(b) Kusoma maneno na kuachumia kuchunga senchensi

**Dhifaa dha kufundrishia**: kadi-maneno, kadi za silabu

**Swali ḏaḏisi**: Ineno huchengedhwaye?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaongodhe vanafundi kuchaya silabi kwene maneno
- Vanafunḏi vasome silabi ubavoni. Mwalimu ahakikishe vanafunḏi hudhitamuka silabi hidho kwa usawa.
- Mwalimu avaongodhe kushikanisha silabi kuundra ineno
- Kachika makundri vanafunḏi vachengedhe maneno kuchumia kadi dha silabi.
- Vanafunḏi vaanḏike maneno valoundra kisha vasome kwa sauti
- Vahimidhe vanafunḏi kuanḏika senchensi vakichumia maneno valoundra.

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. samahani
2. radhi
3. pole
4. huyambo
5. asanṯa

# 4 AFIYA – USWAFI WA NVILI

**ISOMO LA KWANḎA**

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: WIMBO KUHUSU USWAFI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kusoma wimbo

(b) Kukariri wimbo

(c) Kujibu maswali

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi giredi 1 ukurasa wa 13.

**Dhifaa dha kufundrishia**: Dhifaa halisi, chati

**Swali ḏaḏisi:** Kwa nini uswafi ni muhimu?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kueledha umuhimu wa uswafi.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vasome shairi kwa sauṯi
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vakariri shairi kwa sauṯi na kwa mahadhi.
- Mwalimu avavoneshe vanafunḏi dhifaa halisi na vachaye maina
- Mwalimu avavulidhe vanafunḏi maswali vajibu

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. Hubika nswaki
2. Mayi na sabuni
3. Huakacha

## ISOMO LA PILI

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

## MAḎA NDRODI: MAṮANSHI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**:

Kusikilia mwisho wa kipindri mwafunḏi awedhe:

(a) Kuchaya shuhuli dha uswafi

(b) Kufurahiya uswafi

(c) Kutaba shughuli dha uswafi

**Marejeleo:** Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 14

**Dhifaa dha kufundrishia:** Dhifaa halisi, michoro, kifaa cha dijitali

**Swali ḏaḏisi**: Hubika nsuaki mara ngapi kwa siku?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kuchaya shuhuli dha uswafi vafanyadho asubuhi kabula kwendra sikuli.
- Mwalimu avashirikishe kujadili michoro ilioko ukurasa wa 14.
- Vaongodhe vanafunḏi kutaba shuhuli mbalimbali dha uswafi
- Mwalimu avahimidhe vanafunḏi umuhimu wa uswafi.

## ISOMO LA CHACHU

## MAḎA KURU: KUSOMA

## MAḎA NDRODI: NGANU

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kusoma nganu kwa ufasaha.

(b) Kujibu maswali

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi, ukurasa wa 16 – 17

**Dhifaa dha kufundrishia**: chati

**Swali ḏaḏisi**: Uswafi una umuhimu gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi kujadili nchoro kiṯabuni ukurasa wa 16.
- Kuvaongodha vanafunḏi kusoma ufahamu kwa sauti
- Avashirikishe kuchambua maneno magumu (mwalimu aandike maneno magumu ubavoni)
- Vaongodhe kujibu maswali alioko kiṯabuni.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Famau
2. Mwanamboe
3. Afia nḏuri

**ISOMO LA IṈE**

**MAḎA KURU: KUSOMA**

**MAḎA NDRODI: DHICHU DHA USWAFI**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kusoma maina a dhichu dha uswafi.

(b) Kufurahia kusoma.

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi darasa la kwanḏa uk 15

**Dhifaa dha kufundrishia**: Dhifaa halisi, kifaa cha kidijitali, michoro kiṯabuni

**Swali ḏaḏisi**: Huchumia nini kuṯana ṉee?

**Uṯaraṯibu ibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vachaye dhifaa dha uswafi.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kujadili dhichu dha uswafi kiṯabu cha vanafundi ukurasa wa 15.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vasome maina a dhichu dha uswafi dhilidhoko kiṯabuni kwa makundri ukurasa wa 15.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

### MAḎA NDRODI: KUPANGA MANENO

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kupanga maneno lli kuchengedha senchensi sawa.

(b) Kufurahia kuchunga senchensi.

Marejeleo: Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 16.

**Dhifaa dha kufundrishia**: Dhifaa halisi, kadi-maneno

**Swali ḏaḏisi**: Harufu kuru huanḏikwa kwapi kweṉe senchensi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi kuchunga senchensi kuhusu uswafi.
- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi kusoma maneno alioko kwenye kadi maneno lli vachunge senchensi sahihi.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi namna a kupanga maneno lli vachengedhe senchensi sahihi kiṯabu cha vanafunḏi ukurasa wa 16.
- Mwalimu aṯaue mwanafunḏi mmoya asome senchensi kwa sauṯi.

**Majibu alopenḏekedhwa**

1. Imi hubika nsuaki

2. Ukitoka chooni nyava

3. Kila nfuma juma hukota ṉee

4. Imi hukacha madowe angu

**ISOMO LA SIṮA**

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

**MAḎA NDRODI: KUṮAFUDHA MANENO KUṮOKA KWA NRABA**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kupacha ineno sahihi kwene nraba

(b) Afurahie kuandika maneno kuṯoka kweṉe nraba.

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 16.

**Dhifaa dha kufundrishia: chati**

**Swali ḏaḏisi** – Nraba ni nini?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu achangulidhe kipindri kwa kuvaeledha nraba ni nini?
- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi vadhichambue na vasome sauṯi kachika nraba.
- Mwalimu avashirikishe vanafunḏi kutafudha maneno kuṯoka kwa nraba.

**Majibu alopenḏekedhwa:**

1. Kunyava
2. Kuṯana
3. Sabuni
4. Mayi

# 5 NYAKATI NA DHIPINDRI

## ISOMO LA KWANḎA

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: DHIPINDRI DHA SIKU**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuchaya dhipindri dha siku

(b) Kuchambua picha dha dhipindri dha siku.

**Marejeleo** – Kiṯabu cha vanafunḏi ukurasa wa 17.

**Dhifaa dha kufundrishia** – Kifaa cha dijitali, picha kiṯabuni

**Swali ḏaḏisi**: Ni dhipindri gani dha siku udhiivadho?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu achangulidhe isomo kwa kueledha ṯafauti a dhipindri na nyakaṯi.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vaangalie picha.
- Vanafunḏi kachika dhikundri vachaye dhipindri dha siku kulingana na picha.
- Mwalimu avaeledhe vanafunḏi dhipindri mbalimbali dha siku.

## ISOMO LA PILI

**MAḎA KURU: KUSIKIDHA**

**MAḎA NDRODI: SIKU DHA JUMA**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuchaya siku dha juma

(b) Kusoma senchensi.

**Marejeleo** – Kiṯabu cha mwanafunḏi, ukurasa wa 18.

**Dhifaa dha kufundrishia**: kalendra, chati.

**Swali ḏaḏisi**: Juma lina siku ngapi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vaimbe siku dha juma.
- Vanafunḏi vachaye siku dha juma.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vadhisome senchensi kwa makundri.
- Mwalimu avavulidhe vanafunḏi maswali kuhusu siku dha juma.

**ISOMO LA CHACHU**

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

**MAḎA NDRODI: NYEDHI DHA MWAKA**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe

(a) Kusoma nyedhi dha mwaka

(b) Kufurahia kusoma nyedhi dha mwaka

**Marejeleo** – Kiṯabu cha mwanafunḏi ukurasa wa 18-19.

**Dhifaa dha kufundrishia** – kalendra, kadi maneno

**Swali ḏaḏisi**: Mwaka una nyedhi ngapi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha:**

- Changulidha kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali ahusianao na nyedhi dha mwaka.
- Mwalimu avavoneshe vanafunḏi kalendra ivaongodhe nyedhi dha mwaka.

- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vasome nyedhi dha mwaka kwa sauti.
- Mwalimu ahitimishe isomo kwa kuvaagidha vanafunḏi vasome nyedhi dha mwaka kimakundri.

## ISOMO LA IṈE

## MAḎA KURU: KUDHUNGUMUDHA

### MAḎA NDRODI: KUCHUNGA SENCHENSI

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kufikia mwisho wa kipindri, mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuchunga senchensi kuchumia nyedhi dha mwaka.

(b) Kufurahia kuchunga senchensi

**Marejeleo** – Kiṯabu cha mwanafunḏi uk. 18

(c) **Dhifaa dha kufundrishia** – kalendra

**Swali ḏaḏisi**: Mwedhi wa mwisho wa mwaka ni gani?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu achangulidhe isomo kwa kuvaagidha vanafunḏi vasome nyedhi dha mwaka.
- Mwalimu aṯoe mfano wa senchensi kwa kuchumia miedhi a mwaka.
- Mwalimu aanḏike senchensi ubavoni.
- Mwalimu avaongodhe vanafunḏi vachunge senchensi vakichumia nyedhi dha mwaka.
- Mwalimu ahitimishe isomo kwa kurekebisha senchensi validhodhichunga.

## ISOMO LA ṮANU

## MAḎA KURU: KUSOMA

### MAḎA NDRODI: SIKU DHA JUMA

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kusikilia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kusoma siku dha juma

(b) Kuchunga senchensi kuchumia siku dha juma.

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi uk wa 18-19.

**Dhifaa dha kufundrishia**: kalendra, kadi-maneno, kifaa cha kidijitali.

**Swali ḏaḏisi**: Juma lina siku ngapi?

**Uṯaraṯibu wa kufundrisha**

- Mwalimu achangulidhe kipindri kwa kuvavulidha vanafunḏi maswali kuhusu siku dha juma
- Mwalimu asome siku dha juma kwa sauṯi ukurasa wa 18, vanafunḏi pia vasome siku dha juma kwa sauṯi ukurasa wa 18-19.
- Vanafunḏi vaṯoe mifano a senchensi akichumia siku dha juma
- Mwalimu avaagidhe vanafunḏi vadhisome senchensi dhilidhoko kiṯabuni uk wa 19 kwa sauṯi.
- Mwalimu avaagidhe vanafunḏi vaangalie michoro uk. 19 na vaeledhe vakivonacho.
- Mwalimu ahiṯimishe isomo kwa kurekebisha maeledho a michoro kuṯoka kwa vanafunḏi.

**ISOMO LA SIṮA**

## MAḎA KURU: KUANḎIKA

**MAḎA NDRODI: YADHA PENGO**

**Maṯokeo maalumu ṯarajiwa:**

Kufikia mwisho wa kipindri mwanafunḏi awedhe:

(a) Kuyadha pengo kachika nraba

(b) Kutafudha maina a juma na miedhi kweṉe nraba.

**Marejeleo**: Kiṯabu cha mwanafunḏi 1, uk 20.

**Dhifaa dha kufundrishia**: Kadi maneno

**Swali d̠ad̠isi:** Siku a kwand̠a a juma huichwae?

**Ut̠arat̠ibu wa kufundrisha**

- Changulidha kipindri kwa kuvulidha vanafund̠i maswali kuhusu siku dha juma.
- Mwalimu avaagidhe vanafund̠i vayadhe pengo uk wa 20.
- Mwalimu avavoneshe vanafund̠i namana a kuyadha nraba na avaagidhe vachore nraba.
- Vanafund̠i vat̠afudhe maina a juma na miedhi kwen̠e nraba.

**Majibu alopend̠ekedhwa**

| Yadha pengo: | Nraba |
|---|---|
| 1. Jumapili | Mei |
| 2. Jumachachu | Jumachachu |
| 3. Mei | Aprili |
| 4. Disemba | |
| 5. Hamisi | |